JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

LINDI – JULAI, 2020

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA LINDI YAONYA RUSHWA KATIKA UCHAGUZI MKUU, YAOKOA FEDHA SHS 1,203,393,287/= PAMOJA NA MAGHALA YA NAFAKA KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI, 2020

Ndugu waandishi wa habari,

Mkoa wa Lindi unajumuisha Wilaya Sita (6) ambazo ni Mtama, Manispaa, Kilwa, Nachingwea, Liwale na Ruangwa. Katika Kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2020, Ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Lindi imefanya kazi na kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 Marejeo 2019. Majukumu hayo yalifanywa kupitia madawati mbalimbali likiwemo dawati la Uchunguzi, Huduma za Sheria na Mashitaka, Utafiti, Udhibiti, na Elimu kwa Umma.

Ndugu waandishi wa habari,

Kupitia dawadi la uchunguzi, kwa kipindi cha mwezi April - Juni, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilipokea jumla ya malalamiko 91 kuhusiana na vitendo vya rushwa na mambo mengine yanayoshabihiana na rushwa. Malalamiko haya yalihusu sekta zifuatazo: Kilimo na Ushirika 25, TAMISEMI 21, Mahakama 10, Ardhi malalamiko 5, Jeshi la Polisi 4 , Ujenzi 4, Afya 3, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO’s) 3, Elimu 2, Uvuvi 2, Fedha 1, Bima 1, Siasa 1, Biashara 1, Magereza 1 na Maliasili 1. Malalamiko haya yalifanyiwa kazi katika hatua mbalimbali kwa mujibu wa majukumu ya TAKUKURU

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilifanikiwa kuokoa fedha kiasi cha **sh.1, 203,393,287/=** zinazojumuisha fedha za wakulima wa mazao ya ufuta, korosho, miradi mbalimbali ya maendeleo na kodi ya Serikali.

Pia tumefanikiwa kurejesha katika miliki ya Serikali maghala mawili ya kuhifadhia mazao yaliyoko katika Wilaya ya Nachingwea, moja kwa jina maarufu ”ghala ya kijani” lenye

thamani ya Shs. 204,000,000/= na lingine lipo katika Kiwanja Na.476 Kitalu J linalojulikana kama “ghala la pachani” lenye thamani ya Shs.78,000,000/=.

Kupitia ghala la pachani pekee, Halmashauri ya Wilaya Nachingwea itaweza kupata Ushuru wa Shs.114,000,000/= kwa utunzaji wa ufuta pekee kwa msimu wa 2020/2021, kama mapato ya ndani ya Halmashauri na ni faida kwa Serikali. Aidha tuliweza pia kurejesha katika milki ya wananchi trekta la kijiji cha Chikonji na viwanja viwili ambavyo wajanja walikuwa wamejimilikisha.

Kwa upande wa mashitaka, katika Mwaka wa fedha 2019/2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi imefungua jumla ya kesi mpya 1. Jumla ya kesi 3 zimetolewa hukumu katika kipindi hicho, ambapo TAKUKURU imeshinda kesi moja (1) na kushindwa kesi mbili (2).

Ndugu waandishi wa habari,

Katika kipindi cha mwezi Aprili - Juni 2020, TAKUKURU mkoa wa Lindi kupitia Dawati la Uzuiaji Rushwa ilifuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania (**3,292,435,544.20)**. Miradi hiyo ni hii ifuatavyo:- Ukarabati wa Mradi wa Maji Nyangao – Lindi wenye thamani ya sh. 46,500,000/=, Mradi wa maji wa lipa kwa matokeo (payment for result) - Kilwa wenye thamani ya sh. 1,360,000/=, Manunuzi ya Madawa na vifaa tiba Wilayani Kilwa yenye thamani ya sh. 1,587,221,169.3/=, Ujenzi wa Wodi ya Wazazi Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea - Nachingwea yenye thamani ya sh. 400,000,000/=, Nachingwea District Mosque Road – Nachingwea yenye thamani ya sh.1,243,777,468.7/= na Ukarabati wa Mradi wa Kusambaza Maji Kijiji cha Kitogoro (Rehabilitation Of Mpigamiti Water Supply) – Liwale wenye thamani ya sh. 214,936,426.3.

Ndugu waandishi wa habari,

Katika Mwaka wa fedha kuanzia Aprili - Juni, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendelea kutekeleza malengo yake ya dawati la elimu kwa umma kwa kuwaelimisha wananchi wa makundi mbalimbali na wadau wengine juu ya rushwa na madhara yake kwa mtu mmoja mmoja, jamii, taasisi na Taifa kwa ujumla. TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendesha semina 6, imefanya mikutano ya hadhara 33, maonyesho 2, pia imefanya ufunguzi na uimarishaji wa klabu za wanafunzi za wapinga rushwa 34, vipindi vya TV na Redio 2na Makala 7 zenye jumbe mbalimbali ziliandaliwa katika kipindi hicho.

Ndugu waandishi wa habari,

Katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 ulioanza Julai Mosi 2020, pamoja na majukumu mengine TAKUKURU Mkoa Lindi imejipanga kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati mkoani Lindi ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji, kuchambua mifumo ya ukusanyaji wa kodi na mapato ya Serikali, na kuendelea kuelimisha umma madhara ya rushwa katika uchaguzi hususani Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2020.

Pia, TAKUKURU mkoa wa Lindi inatoa wito kwa wananchi, wanaotarajia kugombea katika nafasi mbalimbali pamoja na wadau wa miradi ya maendeleo katika mkoa wa Lindi kuwa wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kujiepusha na vitendo vya rushwa, kinyume na hapo hatua stahiki zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kutenda makosa.

TAKUKURU mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi wa mkoa huu na kuzishukuru taasisi mbalimbali (za binafsi na za Serikali) kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi yetu. Aidha, tunawaomba waendelee kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya bure ya **113** kwani mapambano dhidi ya rushwa sio ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

Imetolewa na:

Stephen Chami

Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi